# Ufafanuzi wa Mada

# Adhabu ya Kifo

Muhtasari ulioandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## Adhabu ya Kifo inakiuka Haki za Binadamu

Kama ilivyosisitizwa katika Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2015, Haki ya Kuishi ndio haki ya msingi kabisa. Ni haki ambayo haki nyingine zinategemea uwepo wake, na kwa hiyo ni lazima ilindwe. Adhabu ya kifo ni kielelezo sahihi cha ukiukwaji wa haki ya kuishi. Kituo cha Sheria na Haki za Bindamu kimekuwa kikiainisha wazi katika taarifa zake ni kwa namna gani kinafanya kampeni kupinga adhabu ya kifo, kwa kuainisha ni kwa jinsi gani pamoja na kuwa adhabu ya kifo ipo kwenye vitabu vya sheria ya nchi lakini hakujakuwa na utekelezaji wa adhabu hiitangu mwaka 1994.

Haki ya Kuishi inalindwa kikatiba chini ya Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamwaka 1977. Hatahivyo ulinzi huu utolewao na Katiba si ulinzi kamili. Hii ni kwa sababu haki ya kuishi kwa mujibu wa Ibara inaweza kuwekewa mipaka na sheria nyingine za nchi. Katika sheria za Tanzania, adhabu ya kifo imewekwa kama adhabu ya lazima kwa mtu atakayepatikana na hatia ya mauaji na uhaini, chini ya Vifungu vya 39 na 197 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Ili adhabu ya kifo itekelezwe, Rais anatakiwa kuweka sahihi hati ya utekelezaji wa adhabu iliyotolewa na mahakama. Kwa mujibu wa Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muun-

Ujumbe Muhimu: *Adhabu ya kifo inakiuka haki ya msingi ya kuishi nchini. Wakati tukielekea kukomesha adhabu ya kifo kuna hatua muhimu ambazo zinatakiwa kuchukuliwa kama vile kutambua rasmi kuwa nchi yetu imesitisha utekelezaji wa adhabu ya kifo lakini pia kuwepo na adhabu mbadala kwa ajili ya majaji kuamua badala ya kuhukumu adhabu ya kifo.*

Ulinzi wa haki ya kuishi unatolewa pia na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo imeridhiwa nanchi yetu. Miongoni mwa mikataba hii ni Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia (Ibara ya 6) na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na na Haki za Watu(Ibara ya 4). Hata hivyo Tanzania haijatia saini wala kuridhia Mkataba Nyongeza ya pili ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia ambao unazitaka nchi zote wanachama kukomesha adhabu ya kifo.

## Mambo ya Kuzingatia

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua mambo muhimu ya kuzingatia kwa ajili ya kuongeza ulinzi wa haki ya kuishi nchini Tanzania:

### 1. Ufahamu mdogo wa jamii na mawazo mchanganyikojuu ya adhabu ya kifo:

Kuna uelewa mdogo wa jamii juu ya adhabu ya kifo nchini. Kuna mitazamo inayotolewa nchini juu ya kuunga mkono adhabu ya kifo mitazamo ambayo inatokana na kiu ya kulipiza kisasi, Imani za kidini na uzoefu binafsi. Ushuhuda unaonyesha kuwa kuna mawazo mchanganyiko nchini juu ya adhabu ya kifo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2014, zoezi la ukusanyaji wa maoni juu ya Uboreshwaji wa Katiba lilihusisha pia swali juu ya adhabu ya kifo. Kwa mujibu wa maoni hayo asilimia 50% ya wananchi walioulizwa walikuwa na maoni ya kuendelea kuwepo kwa adhabu ya kifo.

### 2. Adhabu ya kifo ni adhabu ya lazima kwa makosa ya mauaji na uhaini:

Sheria imeweka adhabu ya kifo kama adhabu ya lazima kwa watu watakaopatikana na hatia katika makosa ya mauaji na uhaini. Kwa watu watakaopatikana na hatia ya makosa haya hawawezi kuomba kupunguziwa adhabu hii. Hii inaleta ugumu zaidi kwa majaji kutoa adhabu mbadala zaidi ya kutoa adhabu ya kifo.

## 3. Katiba, ufafanuzi wake na sheria za nchi:

Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa ulinzi wa haki ya kuishi chini ya Ibara ya 14 lakini pia ina ulinzi dhidi ya adhabu zisizo za kibinadamu, kikatili na zinazotweza utu chini ya Ibara ya 13 (6)(e). Adhabu ya kifo inakiuka haki ya kuishi; njia ya utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa kunyongwa mpaka kufa ni njia ya kikatili, isiyo ya kibinadamu na inatweza utu. Kwa hivyo basi Kituo cha Sheria na Haki za Bindamu kinaamini kuwa adhabu ya kifo ni adhabu inayokinzana na Katiba ya nchi – kwa kupingana na Ibara ya 14 (ambayo inatoa ulinzi mpana dhidi ya adhabu ya kifo) na Ibara ya 13(6)(e) ambayo inakataza kuwepo na adhabu ambayo ni ya kikatili, isiyo ya kibinadamu na inayotweza utu.

Kwa upande mwingine, Ibara ya 14 ya Katiba imeweka maneno ya "kwa mujibu wa sheria" ambayo yanatoa mwanya kwa sheria nyingine za nchi kuweka mipaka ya ulinzi wa haki ya kuishi. Na ni kwa sababu hiyo basi Sheria ya Kanuni ya Adhabu imeweka uwepo wa adhabu ya kifo nakuifanya Serikali kuwa na utetezi kuwa adhabu ya kifo ipo kisheria.

## 4. Uwepo wa hali isiyo rasmi ya usitishwaji wa utekelezaji wa adhabu ya kifo na kutokuridhiwa kwa mkataba wa nyongeza wa kuzuia adhabu ya kifo:

Pamoja na kuwa adhabu ya kifo bado inatolewa kwa mujibu wa sheria, shirika la Amnesty International linaonyesha kuwa nchi ya Tanzania inachukuliwa kama nchi iliyositisha kwa muda utekelezwaji adhabu ya kifo kwa sababu hakujakuwa na utekelezwaji wa adhabu hii tangu mwaka 1994. Hivyo basi kuna hali isiyo rasmi ya kusimamishwa kwa utekelezaji wa adhabu ya kifo. Amnesty International inaichukulia nchi ya Tanzania kama "nchi iliyo katika mchakato wa kufuta adhabu ya kifo kivitendo." Hatahivyo, bila kuweka rasmi hali ya kuwa nchi imesitisha utekelezaji wa adhabu hii, adhabu ya kifo inaweza kutekelezwa wakati wowote ule.

Kuna suala muhimu pia la kutokuridhiwa kwa mikataba ya kimataifa juu ya ukomeshaji wa adhabu ya kifo. MkatabaNyongeza ya piliya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia unakomesha kabisa adhabu ya kifo. Hatahivyo nchi ya Tanzania haijasaini na wala kuridhia Nyongeza hii ya pili ya Mkataba huu wa Kisiasa na Kiraia.

### 5. Ufahamu finyu wa hali ya wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo:

Inaonekana kuwa kuna takwimu za idadi ya watu wanaohukumiwa adhabu ya kifo kila mwaka kama inavyoainishwa kwenye kielezo namba 1. Hatahivyo, hakuna takwimu zinazooonyesha hali waliyonayo wafungwa waliohukumiwa adhabu hiyo ya kifo. Kumekuwa na urasimu sana wa kupata vibali na ruhusa ya kuwafikia wafungwa hawa kwa ajili ya kuainisha hali yao ya kisaikolojia lakini pia na kuwapatia msaada wa kisheria.




Kielelezo 1. Idadi ya Wafungwa Waliohukumiwa Adhabu ya Kifo kati ya Mwaka 2014-2015 (Chanzo: Taarifa ya Haki za Binadamu yam waka 2015)

## Ujumbe Muhimu

### 1. Kuboresha Ufahamu wa Jamii:

Kuna fursa ya kuboresha ufahamu wa jamii juu ya adhabu ya kifo. Ni muhimu kwa wananchi kuelewa kuwa adhabu ya kifo ni adhabu inayokiuka haki ya kuishi ambayo inalindwa kikatiba na kimataifa kwa mikataba mbalimbali. Zaidi ya hayo wananchi wanatakiwa kuelewa kuwa kuna adhabu mbadala ya adhabu ya kifo, kama vile kifungo cha maisha. Ni muhimu pia kuelewa kuwa adhabu ya kifo sio ufumbuzi wa tatizo la mauaji yanayotokea nchini. Viongozi wa kidini wanasauti kubwa ya kuweza kubadili mawazo ya jamii, na wana wajibu wa kusaidia ulinzi wa haki ya kuishi kwa njia ya kufanya utetezi. Wadau wengine muhimu ni waangalizi wa haki za binadamu walioko nchi nzima ambao wanaweza kuchukua jukumu muhimu la kuieleza jamii juu ya umuhimu wa kukomesha adhabu ya kifo.

### 2. Tukielekea katika kukomesha kabisa adhabu ya kifo, kuna mambo ya mara moja ambayo yanaweza kufanywa ili kulinda haki ya kuishi:

i. **Adhabu mbadala:** Hii ni hatua muhimu sana ya mwanzo kuelekea kwenye kukomesha adhabu ya kifo. Majaji wanahitaji kupewa uwezo wa kutoa adhabu mbadala ya adhabu ya kifo. Serikali na Bunge wanatakiwa kuangalia uwezekano wa kubadilisha sheria ili kuwe na adhabu mbadala kwa watu walioptikana na hatia ya kufanya mauaji na uhaini.

ii. **Kutambulika rasmi kwa usitishwaji wa utekelezaji wa adhabu ya kifo:** Serikali lazima itambue kuwa kuna hali ya kusitishwa kwa utekelezaji wa adhabu ya kifo, na hali hii inatakiwa kutambulika rasmi. Kama sehemu ya mchakato, watu waliohukumiwa adhabu ya kifo wanatakiwa adhabu zao zibadilishwe na kuwa adhabu za kifungo cha maisha, hasa wale ambao wamekuwa magerezani kwa kipindi kirefu zaidi bila kujua hatma ya maisha yao. Kutambulika rasmi kwa usistishwaji wa utekelezaji wa adhabu ya kifo kunasaidia mambo yafuatayo:

- Kusitisha utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa nchi ambazo hazijakomesha utekelezwaji wake.
- Kuweka marufuku ya kurudishwa kwa adhabu ya kifo kwa nchi ambazo zimekwisha komesha adhabu ya kifo.
- Kupunguza idadi ya watu waliohukumiwa adhabu ya kifo.

### 3. Ulinzi wa Haki ya Kuishi uwe kamili na madhubuti:

Ibara yoyote ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatakiwa kuwa imara, bila kuwa na vifungu vinavyonyang'anya haki kwa upande wa pili. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria na Katiba inatakiwa kuangalia njia ya kuhakikisha kuwa michakato ya kuboresha Katiba inahusisha kuhakikisha kuwa ulinzi wa Haki ya Kuishi unakuwa kamili.

### 4. Mikataba ya kimataifa isainiwe na kuridhiwa:

Tanzania inatakiwa kusaini na kuridhia Mkataba Nyongeza ya pili ya Mkataba wa Haki za Kisiasa na Kiraia ambao unakomesha adhabu ya kifo. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inatakiwa kuhakikisha kuwa Bunge linaridhia mkataba huu wa nyongeza.

### 5. Taarifa zitolewe juu watu waliohukumiwa adhabu ya kifo:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatoa wito kwa Idara ya Mahakama kuhakikisha kuwa wadau wa haki za binadamu wanapewa fursa ya kuwafikia wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo ili kuangalia hali yao. Hali halisi ya wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo inatakiwa itolewe kwa wananchi ili wananchi wapate ufahamu juu ya dahabu ya kifo.

Idara ya Magereza inatakiwa kuwa na taarifa za wafungwa hawa muda wote na zilizoboreshwa. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inatakiwa kuhakikisha kuwa Idara ya Magereza inatoa nafasi ya kupatikana kwa taarifa za wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo ili taarifa hizo na hali ya wafungwa hao ziweze kuhakikiwa na asasi za kiraia na wadau wengine. Hii ni muhimu sana ili kuelewa idadi kamili na hali ya wafungwa hawa. Kwa sasa hakuna nyenzo huru ya kuthibitisha vilelezo vinavyohusu wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo. Kwa hivyo basi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatoa wito kwa Idara ya Magereza na Wizara ya Mambo ya Ndani kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kuweza kuwafikia wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo ili kuweza kuwa na usimamizi huru wa hali yao.

Agosti 2016

UKaid
from the British people

Facilitated by UHAKIKI Project; a project funded with UK aid from the UK government

LHRC is a non-governmental organisation with core funding from the Royal Norwegian Embassy and the Embassy of Sweden